

Hatua ua tisa: Kutia chumvi



Kukaanga na mafuta

- Tia korosho kwenye mafuta ya mboga yanayochemka kwa dakika moja mpaka ziwe hudhurungi kabisa.
- Mwaga korosho kwenye besheni iliyo na kitambaa cha aina ya pamba na unyunyizie chuumvi.
- Lowesha mafuta yaliyosalia na uziache zipoe ndiposa zitayarishwe kwa kusafarishwa.

Hatua ya kumi: Kufungua Korosho tayari kusafirishwa

- Tia kwenye vijisanduku visiyo ingiza hewa zilizovikwa na karatasi ya *aluminium*.
- Korosho zilizo fungwa vyema zinaweza kukaa kwa muda wa zaidi ya mwaka mmoja.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 5781 I, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Wtatayarishaji:

Pole, F.N. na Muniu, F.K

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo,

KARI Mtwapa

S.L.P. 16-80109, MTWAPA

Simu: (041) 486207/485842


Nukulishi: (041) 5486207

Baruapepe: karimtw@wananchi.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 69 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Tayarisha korosho upate hela



Utangulizi

Korosho ni mmea muhimu wenye manufaa ya kifedha katika pwani ya Kenya. Mahitaji ya njugu zilizoandaliwa yanazidi nchini na ngámbo na hii inawapa wakulima fursa ya kujinufaisha kifedha.

Maandalizi

Hatua ya kwanza: Kusafisha kwa mwanzo

Pitisha korosho kwenye kichungi cha milimita 10 au mtungi ulio na mashimo ili kutoa vifaa vigeni.

Hatua ya pili kutia unyevu

Twika korosho kwenye sakafu inayoteremka na ufunike kwa gunia lililolowaa hadi ziwe na unyevu kiwango cha asilimia 16.

Hatua ya tatu: Kukaanga

- Tia korosho kwenye kikapu cha waya.
- Tia kikapu chenye korosho ndani ya maji maji inayotolewa kwenye ganda la korosho ambayo inachemka kwa muda wa dakika 4 hadi 5. Hii CNSL inayopatikana kutoka kwa korosho hutolewa na kutiwa kwenye mtungi.



Kuosha na mafuta moto

Hatua ya nne: Kukausha

Mwaga korosho zenye rangi ya hudhurungi kwenye kitira na ufunike ganda ya korosho iliyochemka usiku kucha ili kuondoa iliyobakia.

Hatua ya tano: Kubandua funiko la juu

Unaweza kutumia mkono au mashine inayoendeshwa na mkono ya kutoa.

i) Kubandua na mkono

- Wekelea korosho kwenye jiwe tambarare huku umbo la figo likiangalia juu.
- Katanisha katikati ukitumia fimbo.

ii) Kubandua ukitumia shellers

- Weka korosho kwenye visu vyenye umbao la njugu na ukate ganda huku ukihakikisha *kernel* hajaguswa.
- Uwezekano wa kupata korosho zikiwa hazijaharibika ni asilimia 90.

Hatua ya sita: Kukausha

Unaweza kukausha kwa kutumia kikaushaji kitumiacho jua (*solar drier*) au kwenye nyumba ilivyoinuliwa. Tandaza mbegu kwa wepesi kwa muda wa masaa 12 kwenye joto la nyusi 35 hadi 40 ili kupunguza unyevu kutoka asilimia 6 hadi 3.

Hatua ya saba: Kuchambua


- Bingirisha mbegu kwenye mikono ili kutoa maganda.

- Maganda yasiyotolewa na mkono hutolewa na kisu cha mti.



Kuchambua

Hatua ya nane: Kuteua



i) Korosho



ii) Nzima

- Chagua korosho nzima kutoka kwenye zilizovunjika.
- Unaweza kuteua korosho za kiasi tofauti pia.